

# TANGAZO



## **YAH: MAOMBI YA UJUMBE BODI YA HUDUMA ZA AFYA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kondoaa anatangaza nafasi za wajumbe wa Bodi ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya kwa mkaazi yejote wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoaa

### **Nafasi za wajumbe zilizo wazi ni kama ifuatavyo:**

1. Wawakilishi wa watumiaji huduma za Afya (Jamii) – nafasi 4 (Me – 2 Ke - 2)
2. Mwakilishi kutka watoa huduma za Afya kwa faida (Private) – nafasi (1)
3. Mwakilishi kutoka watoa huduma binafsi bila faida (Voluntary Agency) – nafasi (1)

### **Sifa za Waombaji:**

- Awe na umri wa kati ya miaka 25 – 70.
- Awe ni raia wa Tanzania (sharti hili si lazima kwa waombaji kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali).
- Awe na Elimu ya Sekondari na kuendelea.
- Asiwe kiongozi wa Chama chochote cha siasa au mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya Kondoaa
- Awe mwanachama hai wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na zifungashwe na vivuli (photocopies) za vyeti vya masomo na mafunzo aliyonayo mwombaji. Maombi yapitishwe na Kamati za Maendeleo za Kata kisha yatumwe au kuleta kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya Kondoaa,  
S.L.P 1,  
**Kondoaa**

**Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 15 OCTOBER, 2017 saa 9:30**  
Alasiri

**MWL.FALESY MOHAMED KIBASSA**  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
**KONDOA**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KONDOA**

# HALMASHAURI YA WILAYA KONDOA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

WILAYA YA KONDOA  
FAX/ SIMU 0262360313  
E – MAIL ded@kondoadc.go.tz

S.L.P 1,  
KONDOA .



---

KUMB.NA.KDC/M.10/13 VOL.11/49

15. 09. 2017

MTENDAJI WA KATA  
KATA YA .....  
S.L.P 1,  
**KONDOA**

YAH: TANGAZO LA KUGOMBEA NAFASI ZA UJUMBE WA BODI YA AFYA WIALAYA YA KONDOA


Tafadhalii rejea mada tajwa hapo juu,

Mwongozo wa uundaji na Uendeshaji wa Bodi za Huduma za Afya ya Halmashauri na Kamati za Usimamizi za Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati Nchini Tanzania wa mwaka 2013, imekupa jukumu wewe mtendaji wa kata kutoa tangazo kwa nafasi za wajumbe wa **BODI YA AFYA YA WILAYA**.

Kwa barua hii unatakiwa kutoa Matangazo na kuhamasisha wananchi wa maeneo yako kuomba nafasi za uwakilishi wa ujumbe wa Bodi ya Afya Wilaya.

Pamoja na barua hii tangazo linalotoa maelekezo yote limeambatanishwa.

Nakutakia utekelezaji mwema.

  
MWL.FALESY MOHAMED KIBASSA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**KONDOA**

**MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KONDOA**